

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM**

**MAOMBI YA MAREJEO NA. 590/2019**

**BAINA YA**

**RADAR LIMITED.....MLETA MAOMBI**

**NA**

**JIMMY MAGYOMBO NA WENZAKE 4.....MJIBU MAOMBI**

**HUKUMU**


*Tarehe ya mwisho ya Amri: 16/03/2021*

*Tarehe ya Hukumu: 30/03/2021*

**Z. G. Muruke, J.**

Jimmy Magyombo na wenzake 4 walijajiriwa na Radar Limited katika nyakati na tarehe tofauti, waliachishwa kazi siku moja kufuatia mleta maombi kukosa kazi ya kuwapa baada ya kukosa Zabuni Stat Oil Tanzania.

Rada Limited waleta maombi walikuwa wakihudumia Stat Oil Tanzania kwa kuwapelekea madereva waliokuwa wamewaajiri, wajibu maombi wakiwa moja wa madereva hao. Baada ya kutoridhika na upunguzwaji huo, walifungua shauri la kazi Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Julai, 2015. Rada Limited waliweka pingamizi la awali na baada ya kusikilizwa pande zote, ombi la akina Jimmy Magyombo na wenzake liliondolewa kwenye orodha ya mashauri (Struck out) na kupewa siku 14



kufungua shauri upya. Uamuzi huo ulitolewa tarehe 31/03/2016 kwenye mgogoro Kumbukumbu nambari CMA/DSM/KIN /R.245/15.

Kutokana na hukumu iliyoambatanishwa kwenye marejeo haya, inaonekana wajibu maombi walifungua mgogoro namba CMA/DSM/KIN /R.1221/16/129, baada ya kusikilizwa pande zote, mleta maombi Radar Limited, aliamriwa kuwalipa wajibu maombi watano (5) shilingi 3,522,381 kila moja, kwa ujumla shilingi, 17,611,905 (Milioni kumi na saba laki sita kumi na moja elfu mia tisa na tano). Uamuzi huo haukumridhisha mleta maombi, hivyo alifungua marejeo haya akiitaka Mahakama kufanya mapitiao, na kufuta uamuzi na tuzo ya Tume. Usikilizwaji ulikuwa kwa njia ya maandishi. Mwakili wa pande zote mbili walikamilisha majumuisho. Kwa sababu ambazo nitazieleza baadaye sintozungumzia hoja za msingi. Ikumbukwe kwamba, (i) Waleta maombi walifungua mgogoro wa mwanzo kumbukumbu nambari CMA/DSM/ KIN/R.243/15 ambao uliondolewa (struck out) tarehe 31/03/2016.

- (ii) Hukumu inayolalamikiwa ni tuzo ya mgogoro kumbukumbu nambari CMA/DSM/KIN/R.1221/16/129 ulisomwa tarehe 24 mwezi Mei, 2019 na kama ilivyoombwa kwenye Notisi ya marejeo ya tarehe 05/07/2019.
- (iii) Mahakama wito wa tarehe 19/07/2019, iliitisha jalada la Tume kumbukumbu nambari CMA/DSM/KIN/R.1221/16/129.
- (iv) Jalada tulilonalo la tume ni kumbukumbu nambari CMA/DSM/KIN /R.243/15 ambalo kesi iliondolewa (struck out).

Kwa mantiki hiyo basi, marejeo haya hayana mwenendo stahiki. Mahakama haina mwenendo sahihi wa kuweza kuangalia ushahidi na



vielelezo stahiki, ili kuvipitia na kutoa uamuzi juu ya uamuzi na tuzo inayolalamikiwa. Bila kujua kilichojiri Tume, kwa kuangalia ushahidi na vielelezo, itakuwa ni sawa na kukalia tawi lisilokuwa na shina. Hivyo ni wazi kwamba marejeo haya yameambatana na kumbukumbu (proceedings) za tume zisizo sahihi.

Hakuna namna nyingine zaidi ya kuyaondoa marejeo haya kwenye orodha ya mashauri yaliyopo kwenye kumbukumbu za Mahakama. Kwa minajili ya utendaji haki (interest of justice) marejeo nambari 590/2019 yemeondolewa kwenye kumbukumbu za Mahakama hii, hata hivyo mleta maombi amepewa muda wa siku thelathini (30) kufungua marejeo mengine ikiwa ni pamoja kumbukumbu zake sahihi.

  
Z.G. Muruke

**JAJI**

30/03/2021

Hukumu hii imetolewa na kuthibitishwa leo mbele ya Flavian John kwa niaba ya mleta maombi, na akishika mikoba ya Gasper Thulway.

  
Z.G. Muruke

**JAJI**

30/03/2021